# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA NGOME

# (NGOME SACCOS LTD)

**DSR 991**

# SERA YA WASTAAFU

**TOLEO LA 1: 2020**

# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA NGOME

# (NGOME SACCOS LTD)

**DSR 991**

## SERA YA WASTAAFU

**TOLEO LA 1: 2020**

**YALIYOMO**

HISTORIA YA CHAMA....................................................................4

SABABU ZA KUWA NA SERA..........................................................4

MAREJEO YA SHERIA.....................................................................5

FAIDA ZA KUWA NA SERA ...........................................................5

NAFASI YA UWAKILISHI................................................................6

NAMNA YA KUPATA MWAKILISHI MSTAAFU.................................6

VIONGOZI WA MATAWI.................................................................7

VIKAO VYA WASTAAFU..................................................................7

MAJUKUMU YA VIONGOZI WASTAAFU..........................................7

KAZI ZA WAWAKILISHI WASTAAFU...............................................8

KANUNI ZA JUMLA KWA WAWAKILISHI WASTAAFU.......................9

MAMBO YA KUZINGATIA KWA WAWAKILISHI WASTAAFU..............9

NAMNA YA KUPATA MIKOPO NA UREJESHAJI........................................10

KUPATA TAARIFA ZA CHAMA..................................................................10

WADHAMINI WA MIKOPO.......................................................................10

KUCHANGIA AKIBA...............................................................................11

FURSA KWA WASTAAFU.........................................................................11

HITIMISHO...........................................................................................12

## 1.0 HISTORIA YA CHAMA

NGOME SACCOS LTD yenye nambari ya usajiri DSR 991 ilisajiliwa tarehe 30 April 2007, chini ya sheria ya Ushirika No. 20 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004, kama inavyorejewa na sheria ya sasa ya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013 na kanuni zake. Wanachama wa Ngome SACCOS Ltd wanatokana na fungamanisho (common Bond) ya Maafisa ,Maaskari , Wastaafu pamoja na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wale waliohamia wizara nyingine wakiwa wanachama Hai wa Ngome SACCOS .

## 1.1 SABABU YA KUWA NA SERA HII

Kwa mujibu wa sheria za vyama vya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013, inayosomwa pamoja na kanuni ya 51 ya vyama vya ushirika ya mwaka 2015. Bodi ya chama cha ushirika pamoja na mambo mengine ina wajibu wa kutengeneza SERA mbalimbali ili kukidhi mahitajio ya chama na usimamizi wa rasilimali zake. Kwa mustakabali huu, SERA ya wastaafu itatoa mwongozo kwa wastaafu namna ya ushiriki wao kuhamasisha wastaafu kuwekeza fedha zao pia kujiunga na chama kikamilifu, namna ya kuongeza mapato ya chama na haki yao kama wanachama wengine wanaotimiza masharti haya, kutoa kero na malalamiko miongoni mwa wastaafu.

## 1.2 MAREJEO YA SHERIA

Sera hii imetengenezwa kwa kuzingatia sheria mbalimbali zikiwemo:-

(i) Sheria ya Vyama vya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013.
(ii) Sheria Na 10 ya Huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018
(iii) Kanuni za Huduma ndogo za fedha za mwaka 2019
(iv) Kanuni za Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015
(v) Masharti ya NGOME SACCOS LTD ya mwaka 2007 na marekebisho yake ya mwaka 2018 aya ya 3.2. (Sifa ya mwanachama).

## 1.3 FAIDA YA KUWA NA SERA YA WASTAAFU

Faida ya kuwa na sera hii ni pamoja na kuwatambua wastaafu, kuwa ni miongoni mwa waanzilishi wa Ushirika huu wa Ngome pia kuweka haki sawa kwa wastaafu ambao wanatimiza masharti ya uanachama kama inavyoelekezwa katika Katiba ya chama na sera ya Fedha na Mikopo. Bila kuathiri utangulizi huu, zifuatazo ni miongoni mwa faida ya sera hii:-

(i) Kupata wawakilishi wa chama kwenye Mkutano Mkuu.
(ii) Ushiriki katika kupiga kura na kupigiwa kura.
(iii) Kutoa michango yao juu ya ustawi wa chama.
(iv) Kushiriki katika semina mbalimbali ambazo zitakuwa zinaandaliwa na chama kwa wanachama wake.
(v) Kutoa elimu kwa wastaafu wengine ambao sio wanachama ili waweze kujiunga na chama.
(vi) Kutatua kero mbalimbali za wastaafu ili waendelee kuwa wanachama wenye hadhi sawa na wanachama ambao hawajastaafu.
(vii) Kuzuia wimbi la wastaafu kujitoa.

## 1.4 NAFASI YA UWAKILISHI

Kwa mujibu wa kifungu 1.1(h) cha masharti ya chama, inayosomwa pamoja na SERA ya uwakilishi, wastaafu wanaotokana na fungamanisho la NGOME SACCOS LTD (ambao ni Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma, Wastaafu wa Wizara ya Ulinzi na JKT na Watumishi wa Umma waliohama kwenda wizara nyingine wakiwa ni wanachama wa NGOME SACCOS LTD). Kwa mantiki hiyo, wawakilishi wa wastaafu kwenye Mikutano Mikuu ya chama, watatokana na fungamanisho hili angalau kila kundi litoe wawakilishi wawili, ambapo jukwaa la Mkutano Mkuu litawakilishwa na wastaafu kumi na nane (18). Aidha, Uwakilishi wa wastaafu utatokana na mkao wa kikanda na brigedi ambapo kwa sasa ni tisa (9).

## 1.5 NAMNA YA KUPATA MWAKILISHI MKUU WA WASTAAFU

a. Wawakilishi wastaafu, watatokana na wanachama wastaafu, wanaotimiza masharti ya uanachama kwa kuwachagua walioomba nafasi hizo au kwa namna nyingine itakavyokuwa inapendekezwa na Mkutano Mkuu.
b. Kutakuwepo na muwakilishi mkuu wa wastaafu , ambaye atachaguliwa katika wanachama wastaafu.
c. Mwakilishi wa wastaafu atachaguliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu na atawajibika kwa wanachama wastaafu , pia atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu(3). Mwakilishi wa wastaafu anaweza kusimamishwa na Mkutano Mkuu kwa sababu za kushindwa kutekeleza majukumu yake. Taarifa ya kusimamishwa kwake itapelekwa katika Mkutano Mkuu unaofuata kwa ajili ya maamuzi ya mwisho.

### 1.5.1 VIONGOZI WA MATAWI/ KANDA WASTAAFU

a. Matawi ya chama yatakuwa na wastaafu watakaochaguliwa katika Mkutano Mkuu ambao kati yao ndiyo atapatikana Mwenyekiti na katibu

b. Mwenyekiti ndiyo msemaji mkuu wa tawi/kanda na katibu atakuwa mtendaji wa kazi tawini/ kanda.

### 1.5.2 VIKAO VYA WASTAAFU

a. Kutakuwa na vikao vya wastaafu viwili kabla na baada ya Mkutano Mkuu wa mwaka wa chama kufanyika.

b. Kikao cha maandalizi ya Mkutano Mkuu, kikao hiki kitajadili mambo yafuatayo:-

   i. Kuthibitisha (akidi) mahudhurio.
   ii. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Mkuu uliopita.
   iii. Kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya chama na kutoa maoni ya namna bora ya uendeshaji wa shughuli za chama.
   iv. Kuandaa dondoo za kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu.
   v. Kuchagua wastaafu amabo watahudhulia Mikutano Mikuu ya chama kwa niaba yao. Uchaguzi utaratibiwa na viongozi wa chama.

### 1.5.3 MAJUKUMU YA VIONGOZI WASTAAFU

a. Mwenyekiti wa tawi/kanda ni kiongozi na muwakilishi wa wastaafu wanachama wote kwenye tawi/ kanda.

b. Mwenyekiti atachaguliwa na wanachama katika tawi/ kanda.

c. Ataongoza tawi/ kanda kwa kipindi cha miaka mitatu (3) isipokuwa anaweza kuachishwa na uongozi wa wastaafu na wanachama wastaafu, kabla ya kipindi hicho na uchaguzi mwingine kufanyika endapo atakuwa na makosa au anakabiliwa na makosa.

### 1.5.4 KAZI ZA WAWAKILISHI WASTAAFU

a. Kupitia, kujadili na kupitisha bajeti ya chama ya mwaka.
b. Kuhamasisha wastaafu ambao sio wanachama kujiunga na chama.
c. Kusimamia ujazaji wa fomu za taarifa za mwanachama mstaafu kwa ajili ya kumbukumbu katika daftari la wanachama.
d. Kutoa taarifa katika ofisi ya chama ya mambo mbalimbali yanayotokea katika tawi/ kanda kwa wakati kwa hatua zaidi.
e. Kuhakikisha wanachama wastaafu waliolipwa hisa zao katika tawi/ kanda , wanakabidhi cheti cha hisa kwa muwakilishi na kirudhishwe ofisini.

### 1.5.5 WAJIBU WA WAWAKILISHI WASTAAFU

a. Kuwa kiungo katika chama.
b. Kuwa watetezi wa wanachama wastaafu na chama.
c. Kutunza taswira ya chama.
d. Kuunda timu moja na viongozi wa juu katika utendaji kazi wa chama kwa wastaafu.
e. Kujenga na kuimarisha mshikamamno baina ya wanachama na viongozi wa juu.
f. Washauri wa viongozi wa chama.
g. Kuwa mfano bora.
h. Kuhudhuria Mkutano Mkuu.
i. Kujua taratibu zinazotumika katika kulipa mafao, madai mbalimbali ya wanachama wastaafu.
j. Kutunza data, kumbukumbu katika kila kanda.
k. Kuhamasisha wastaafu wasio wanachama kujiunga na chama.
l. Na wale wanachama kuwapa elimu wasaafu wasio wanachama kujiunga na uwanachama.

### 1.5.6 KANUNI ZA JUMLA KWA WAWAKILSHI WASTAAFU

a. Kujitoa muhanga kutumikia wanachama wastaafu
b. Uadilifu
c. Kufanya maamuzi kwa kuzingatia taarifa za wastaafu katika tawi/kanda
d. Uwajibikaji
e. Uwazi
f. Ukweli
g. Msimamo

### 1.5.7 MAMBO YA KUWA MAKINI NAYO WAWAKILISHI WASTAAFU

a. Viwango na mwenendo
b. Tabia za ushirika
c. Kufanya uamuzi kiushirika
d. Mamlaka na ukomo wake
e. Sifa za mwanachama mstaafu
f. Maamuzi kuhusu kodi ya pango/ofisi endapo zitatengenezwa
g. Mgongano wa maslahi
h. Masuala ya fedha
i. Matukio maalum
j. Kupima mafanikio ya chama kwa upande wa wastaafu
k. Matakwa ya wanachama wastaafu.
l. Uhusiano wa Bodi, Menejimenti na Wastaafu.

## 1.6 NAMNA YA KUPATA MIKOPO NA KUREJESHA

Changamoto ambayo imekuwa inajitokeza kwa wastaafu ni kuwa na mashaka katika urejeshaji wa mikopo. Ili kuepuka changamoto hizo, mstaafu atakopa mikopo yake kama inavyoelekezwa kwenye sera ya mikopo na sera ya fedha. Baada ya mkopo mstaafu anaweza kurejesha kwa kufuata utaratibu kama ulivyo kwenye Sera ya Mikopo kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia kiinua mgongo chake HAZINA.
(ii) Kupitia Bank standing order
(iii) Kurejesha fedha taslim kwa mwanachama aliyeweka dhamana ya mali isiyohamishika.
(iv) Kwa njia nyingine yoyote ambayo Kamati ya mikopo itaona inafaa na kuishauri Bodi kwa ajili ya kuridhia.

## 1.7 KUPATA TAARIFA ZA CHAMA

Wastaafu, watapata taarifa za maendeleo ya chama na haki zao kupitia kwa wawakilishi wao wastaafu, website, vikosi na Makao Makuu ya Chama na njia nyingine yoyote iliyosahihi.

## 1.9 WADHAMINI WA MKOPO

Mikopo ya mwanachama mstaafu itadhaminiwa na mwanachama wa Ngome SACCOS Ltd anayetimiza masharti ya uanachama kama inavyoelekezwa katika Sera ya mikopo ya chama.

## 2.0 KUCHANGIA AKIBA

Akiba ya kila mwezi kwa mstaafu itachangiwa kwa hiari na kwa mujibu wa kifungu cha 3.1© cha masharti ya chama na kama inavyoelekezwa katika sera ya Fedha ya chama. Mstaafu anaweza kutoa michango ya kila mwezi kupitia:-

(i) Kwenye kiinua mgongo cha kila mwezi kupitia HAZINA kuja Ngome SACCOS Ltd.

(ii) Kuwasilisha pesa taslim kwenye ofisi ya Makao Makuu ya chama Mwenge Mlalakuwa.

(iii) Kulipa kwenye Benki **CRDB** akaunti Namba **01J100557300**na **NMB** akaunti Namba **22210003433**na kuwasilisha risiti Makao Makuu ya NGOME SACCOS LTD Mwenge Mlalakuwa.

(iv) Kwa njia nyingine yoyote itakavyopendekezwa na Bodi.

## 3.0 FURSA KWA WASTAAFU

(i) Upendeleo utolewe kwa wastaafu kupata fursa ya kuajiriwa NGOME SACCOS LTD pamoja na kampuni yake tanzu ya NGOME HOLDING GROUP LTD kwa wale watakaoonekana wana ujuzi na hitajio linalokuwepo.

(v) Kubuni bidhaa zingine zitakazokwenda sambamba na hitajio la Chama.

## 4.0 HITIMISHO.

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya Ngome SACCOS na Kamati ya Usimamizi iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua yenye kumbukumbu Na. MA.82/309/20/14 ya tarehe 05 AGOSTI, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

Mwenyekiti

Katibu

NGOME SAVING AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED
NGOME SACCOS LTD
REG. DSR 991
P. O. Box 35923
DAR ES SALAAM

TANZANIA
Approved this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies